

HABARI LEO UK 5.

# * Wauza nyama buchani wahadharishwa *

**Na Sifa Lubasi**

OFISA Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna amewataka wafanyabishara wa machinjio ya kuku na wauza nyama kwenye mabucha, kufanya kazi zao kwa umakini ili kuzuia mlipuko wa magonjwa.

Yuna alisema hayo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara hao kutokana na ukaguzi alioufanya kwenye machinjio ya kuku na mabucha ya kuuzia nyama yaliyopo katika masoko ya jiji hilo.

Aliwataka kuhakikisha machinjio hayo yanakuwa katika mazingira safi kwa muda wote.

Alisema baadhi ya machinjio ya kuku na mabucha, yana mazingira ambayo siyo rafiki katika suala la usafi, hivyo ni muhimu wakajihadhari na milipuko ya magonjwa yanayoweza kujitokeza kutokana na suala hilo.

"Mjihadhari na magonjwa yanayoweza kujitokeza kutokana na mazingira mnayofanyia biashara zenu, hapa tatizo likitokea siyo nyinyi tu bali hata kwa wateja wenu pia wanaweza kujikuta wakikumbwa na ugonjwa," alisema.

Alisema bado kuna changamoto kwa baadhi ya wafanyabiashara ndogo, kutozingatia usafi kwenye maeneo wanayofanyia biashara zao, hali ambayo imekuwa ikisababisha kuwepo kwa takataka na harufu kali ya uchafu.

Ofisa huyo wa masoko aliwataka wafanyabishara ndogo maarufu wamachinga, kufuata kanuni na sheria zinazoelekezwa na jiji kwa kutofanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi, yanayohatarisha maisha na bidhaa zao..

Akizungumza na wafanyabishara kwenye masoko yaliyovamiwa na wamachinga, aliwataka kutofanya shughuli katika sehemu ambayo siyo rafiki kwa upande wao.

Alisema bado kuna changamoto kwa baadhi ya wamachinga kupanga bidhaa zao maeneo yasiyo rafiki kwao na kwa wateja wao na kusababisha adhaa kubwa inayoweza kujitokeza.

"Wengi hukimbilia kupanga bidhaa kandokando ya barabara maeneo ambayo hutumika kupita magari na pikipiki, hali hii inaweza kusababisha ajali na pia uharibifu wa bidhaa zao na hata kwa maisha yao ikiwemo na wateja wanaonunua bidhaa hizo," alisema.

Alisema jiji hilo halitakuwa tayari kuwaona baadhi ya wamachinga, wakikiuka maelekezo yaliyotolewa ya ufanyaji biashara.

Alisema jiji hilo litaendelea kutoa elimu, ili sheria na utaratibu uweze kuzingatiwa na kuheshimiwa kwa pande zote mbili.

Aliwataka wafanyabiashara hao kushirikiana na halmashauri ya jiji pale wanapogudua kuna baadhi yao wamekiuka maelekezo kutoka ngazi husika, kama vile kuvamia maeneo yaliyotengwa kwa ajili ya shughuli za kiserikali na kuweka vibanda vya biashara.

Scanned with CamScanner

HABARI LEO UK 19.

# Kiwanda cha Ngozi Karanga kuingiza bil 80/- kwa mwaka

**Na Nakajumo James, Moshi**

MRADI wa kiwanda cha bidhaa cha ngozi cha kimataifa cha Karanga, unatarajia kuingiza mapato Euro milioni 29.9 (zaidi ya Sh bilioni 79.7 kwa mwaka).

Aidha, zaidi ya wafanyakazi 7.000 wakiwemo wa kudumu 3,000 na ajira za muda maalumu 4,000 watanufaika kutokana na shughuli za uzalishaji kwenye mnyororo wa thamani.

Meneja wa kiwanda hicho, Omary Masoud alieleza hayo kwa timu ya makatibu wakuu wa wizara nne, ambazo kwa namna moja au nyingine zinanufaika moja kwa moja na kuanza na uendeshaji kiwanda hicho.

Makatibu wakuu hao ni wa Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge, Kazi, Ajira na Wenye Ulemavu), Andrew Massawe, Katibu Mkuu Mifugo na Uvuvi (Sekta ya Uvuvi), Profesa Elisante Ole Gabriel, Katibu Mkuu wa Viwanda na Biashara, Profesa Riziki Shemdoe na Katibu Mkuu Mambo ya Ndani ya Nchi, Christopher Kadio na Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), Hosea Kashimba.



Masoud alisema kiwanda kitazalisha jozi 4,000 za viatu kwa siku sawa na jozi milioni 1.2 kwa mwaka, jozi za soli za viatu 800,000 mpaka milioni 1.2 kwa mwaka, kuchakata ngozi futi za mraba milioni 13 kwa mwaka na kwamba asilimia 60 zitatumika kiwandani na asilimia 40 soko la ndani na nje ya nchi.

"Pamoja na bidhaa hizo, pia tutatengeneza mikoba ya wanawake na wanaume, mikanda, makoti ya aina zote, mifuko ya makochi ya magari, mifuko ya kubebea silaha, mipira ya michezo ya aina mbalimbali na bidhaa nyingine za ngozi," alisema meneja huyo.

Makatibu wakuu walishiriki usimamizi wa ufungaji wa mitambo ya kisasa kwenye kiwanda hicho, kinachojengwa kwa gharama ya zaidi ya Sh bilioni 136. Kinatarajiwa kuanza kazi rasmi Oktoba mwaka huu.

Naibu Katibu Mkuu Wizara ya Viwanda na Biashara, Ludovicky Nduhiye alisema kuna haja ya serikali kutumia fedha za mfuko wa ngozi ili kuboresha mazao yatakoanayo na mifugo.

Mradi huo unaendeshwa kwa ubia kati ya PSSSF na Jeshi la Magereza, kwa usimamizi wa kampuni tanzu ya Karanga Leather Industries (KLICL).

kuunganisha nguvu

...ibu

...ikisha tuna-
...etu nchini."
...ziri wa Kili-
..., akikabidhi
...kwa ajili ya
... mbegu wa
...hini, alisema
...o hilo kuwa
...kakati.
... kwa sasa ni
...a ujenzi wa
...a mvinyo na
...nengi. Kama
...akikisha hili
...awekeza vya
...wa kiwango
...ahitaji ndani
...a.
...ijenzi wa vi-
...changia ku-
...a kuchangia
...a kuongeza



...nyoosha
...delea wa

...2/-

...a Mdhibiti
...a Hesabu
...a 161 kwa
...kwa mwa-
...imia 71 ya
...itatu mfu-
...ri katika
... CAG kwa
... msisitizo
...tofauti na
...o ilipata
...sema.

# Wachinjaji, wenye bucha watakiwa kuzingatia usafi

**Na Peter Mkwavila,**
DODOMA

WAFANYABIASHARA wa machinjio ya kuku na wamiliki wa bucha za nyama katika Jiji la Dodoma, wametakiwa kuzingatia usafi ili kujiepusha na magonjwa ya mlipuko.

Ofisa Masoko wa Jiji hilo, James Yuna, aliyasema hayo jana alipokuwa akizungumza na wafanyabiashara hao baada ya kukagua hali ya machinjio na bucha kwenye masoko mbalimbali ya Jiji la Dodoma.

Alisema kanuni za afya zinapaswa kuzingatiwa kwenye maeneo hayo kwa kuhakikisha yanakuwa safi muda wote.

"Baadhi ya machinjio ya kuku na bucha mazingira yake si rafiki hususan katika suala zima la usafi, hivyo ni muhimu mkachukua tahadhari zote ili kutokumbwa na magonjwa ya mlipuko," alisema.

Yuna pia alisema bado kuna tatizo kwa baadhi ya wafanyabiashara wadogo kutozingatia usafi kwenye maeneo ambayo wanafanyia biashara zao na kusababisha taka kusambaa ovyo.

Aliwataka wafanyabiashara hao kufuata kanuni na sheria za Jiji kwa kutofanya biashara kwenye maeneo yasiyo rasmi.

"Kuna tatizo wamachinga wamekuwa wakipanga bidhaa zao kwenye maeneo yasiyo rafiki wengi wanakimbilia kupanga bidhaa kando kando ya barabara ambayo inatumika kupita magari na pikipiki, hii inaweza kusababisha ajali pia na uharibifu wa bidhaa zao na hata kwa maisha yao," alisema.

Aliongeza: "Pamoja na kuwa na vitambulisho siyo sababu ya kukaidi maelekezo ambayo yapo kwa faida yenu, kinachotakiwa hapa ni kuheshimu na kuepukana na tabia ya kupanga bidhaa kwenye maeneo hatari."

Alisema kuwa Jiji halitakuwa tayari kuwaona baadhi ya wafanyabiashara wanakiuka maelekezo yaliyotolewa katika kufanya biashara.

Scanned with CamScanner

IMANI NATHANIEL



Hakimu

/a
suaji
vatoto
ıwa

RY

/lifupa (MOI)
umu ya wa-
vikubwa na
itaambatana
upasuaji kwa

jana, Mkuu
ano Moi, Pat-
/ito kwa wa-
watoto hao
huduma hiyo

ma kwamba
le cha maa-
lay' kuanzia
eandaa klini-
itoto wenye
gongo wazi,"

katika kliniki
i watapata
na huduma
).
yika katika
jipya la Moi
ambayo ita-
maegesho ya
itengo cha
a Moi.
i na walezi
ahi kwa ajili
pewa tarati-
rama zozote
tiza Mvungi.
iki hiyo pia
lugu na wa-
huduma za

nbi hii im-
a kushiriki-
Azim Dewj,
Catering na
na Mvungi.

UVUVI

# Wadai kanuni mpya za uvuvi zimekimbiza wavuvi baharini

Na CHRISTINA GAULUHANGA -DAR ES SALAAM

MWENYEKITI wa Soko la Kimataifa la Samaki Feri, Mbaraka Kilima, amesema uhaba wa samaki ambao umefanya kupanda bei ya bidhaa hiyo, unatokana na mabadiliko ya kanuni za uvuvi.

Akizungumza na MTANZANIA Dar es Salaam jana, Kilima alisema mabadiliko ya kanuni hizo yamesababisha baadhi ya wavuvi kushindwa kuingia baharini kuvua zaidi ya mwezi sasa.

Alisema hali hiyo imesababisha ndoo moja ya samaki kuuzwa Sh 120,000 na kuendelea tofauti na kipindi cha nyuma.

Kilima aliongeza kuwa kipindi cha nyuma samaki walikuwa wakiuzwa ndoo ndogo Sh 30,000 hadi 40,000 huku wakubwa wakiuzwa Sh 50,000 hadi 70,000 bei ambayo wafanyabiashara wengi waliweza kumudu tofauti na hivi sasa ambapo wengi wanakosa biashara na wateja pia wakiadimika.

"Mabadiliko ya kanuni za uvuvi ambayo yameainisha aina ya nyavu yamesababisha wavuvi wengi kusitisha shughuli hiyo, hali iliyofanya bei ya samaki kuwa juu na wavuvi wengi kukabiliwa na hali ngumu ya maisha," alisema Kilima.

Alisema hata hivyo uongozi wa soko hilo unaendelea na mikakati kadhaa kuhakikisha wavuvi wanarejea baharini na bidhaa hiyo kuendelea kupatikana kwa wingi.

Kilima alisema pia wanaendelea kufanya maboresho ya miundombinu ya soko hilo ili kuondoa changamoto ndogo ndogo zilizopo hivi sasa.

Pia alisema wanaendelea kufanya uhakiki wa wafanyabiashara wa soko hilo ili kufahamu kama huduma zilizopo sasa wananufaika nazo.

Kwa upande wake, mfanyabiashara Sadick Jumanne aliiomba Serikali ikutane na wavuvi hao ili waweze kuelezea changamoto wanazokabiliana nazo hivi sasa.





UCHAGUZI MKUU 20



# Mgombea ubunge awaombea wafugaji mbegu za ng'ombe

**Na SAFINA SARWATT**
-MOSHI

MGOMBEA ubunge wa Viti Maalumu kupitia CCM, Shally Mushi amemwomba Waziri Mkuu Kassim Majaliwa endapo wananchi wa Moshi Vijijini watampa kura katika Uchaguzi Mkuu wa Oktoba, awasaidie kupata mbegu mpya na bora za mitamba ya ng'ombe wa maziwa ili waweze kujiinua kiuchumi.

Shally pia alimwomba Majaliwa kupitia serikali kuwasaidia wananchi kupata mbugu bora za mbuzi wa maziwa na kuku wa kisasa ili kuwawezesha kufuga kisasa kwa lengo la kupambana na umasikini.

Mgombea huyo aliyasema hayo jana, katika mkutano wa hadhara wa uzinduzi wa kampeni za kumnadi mgombea ubunge wa jimbo la Moshi Vijijini, Profesa Patrick Ndakidemi uliofanyikia katika viwanja vya Kibosho Kirima.

Alisema wananchi wa Moshi Vijijini ni wakulima na wafugaji wazuri hivyo wana kila sababu ya kupatiwa mbegu mpya za mitamba ya ng'ombe na mbuzi wa maziwa kukuwa kisasa ili waweze kujiendeleza na kuachana na umasikini.

"Huku kuna akina mama wengi wafugaji wazuri wakiwezeshwa wanaweza kubadilisha maisha ya familia zao kwa kuuza maziwa kuku wa nyama na mayai endapo watawezeshwa," alisema.

Akizungumzia ujenzi wa kiwanda cha viatu na bidhaa zitokanazo na ngozi cha Magereza kilichopo mjini Moshi, alisema kiwanda hicho kikikamilika serikali haina budi kuweka mazingira ya kitoa ajira hamsini hamsini kwa wanawake na wanaume kwani kiwanda hicho kikikamilika kinaweza kutoa ajira zaidi 3000.

Alisema kama ilivyo kwa shirika la reli aliweza kuishawishi na kutoa nafasi kwa wanawake kupata tenda ya kupika vyakula n'a kuiza vinywaji ili waweze kujikwamua kiuchumi.

Naye mgombea ubunge wa Moshi Vijijini, Professa Patrick Ndakidemi aliwaomba wananchi wa jimbo hilo kumchagua kuwa mbunge wao hilo ili aweze kutumia taaluma yake ya kilimo kwa kushirikiana na wadau mali mbali kuleta maendeleo ya wananchi.

-PICHA: HADIJA OMARI



# Dk. M... matu... wan...

**Na GUST...**
-PWANI

MGOMB... la Kibaha... Chama C... Maendel... Michael... matuma... ya Sofu i... kuwa wa... kushugh... kuzipati...

Mtal... jana wal... wananc... wa kam... viwanja... Twende... Sofu Kil...

Alis... Sofu im...

